TOLEO MAALUM LA OKTOBA - DESEMBA 2022

AFYA BULLETIN

# HUDUMA ZA AFYA MAZINGIRA NA USAFI



## KUTOKA KWA VIONGOZI WETU

**"Wakuu wa Mikoa na Wilaya, hakikisheni suala la usafi kwenye barabara kuu zinazounganisha mikoa na wilaya linakuwa endelevu."**

Dkt.Philip Isdor Mpango

# DIBAJI

Huduma za Afya Mazingira na Usafi ni mojawapo ya sehemu nne zinazounda Idara ya Kinga. Sehemu hii inaoongozwa na Mkurugenzi Msaidizi akisaidiwa na Wakuu wa Sehemu ndogo nne.

Sehemu ndogo hizo ni Afya Mipakani, Usalama Mahala pa Kazi, Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira na Sehemu ndogo ya Usalama wa Maji, Chakula na Usafi wa Mazingira.

Aidha, Sehemu hiyo inaratibu miradi miwili; Kampeni ya Kitaifa ya Afya na Usafi wa Mazingira yenye lengo la kuboresha huduma za afya na usafi wa mazingira katika ngazi ya kaya, taasisi na vituo vya kutolea huduma za afya. Mradi mwingine ni udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya.

Sehemu ya afya mazingira na usafi ina majukumu makubwa ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera; kuandaa Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo inayohusu afya mazingira na usafi; kufuatilia na kusimamia pamoja na kuiwezesha Mikoa na Halmashauri katika kutekeleza afua za afya mazingira na usafi. Halikadhalika, kutafuta rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa afua za afya mazingira na usafi nchini.

Lengo la Afya Mazingira na Usafi ni kukabiliana na kudhibiti kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kama vile Ebola, UVIKO 19, Kipindupindu, Kuharisha na magonjwa yatokanayo na athari za kemikali na mionzi kwa kudhibiti visababishi vya afya mazingira na usafi. Aidha, afya mazingira na usafi husaidia kukuza ustawi wa jamii kwa kuweka maeneo yanayozunguka jamii kuwa nadhifu. Afua hii hujumuisha udhibiti wa taka, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, usalama wa chakula maji, usalama wa afya mahala pa kazi, ujenzi wa vyoo bora na matumizi pamoja na tabia chanya za usafi katika jamii.

Kwa mantiki hiyo, jarida hili linalenga kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu afya mazingira na usafi dhidi ya magonjwa kwa kufuata na kuzingatia kanuni za afya ili kudhibiti maambukizi na kuenea kwa magonjwa. Hii itasababisha kupunguza wagonjwa na vifo na hatimaye kukuza uchumi na jamii





**Prof. Abel Makubi**
**KATIBU MKUU - AFYA**


## BODI YA WAHARIRI

### Mwenyekiti

Prof. Abel Makubi
KATIBU MKUU - AFYA

### Wajumbe

Prof. Tumaini Nagu
MGANGA MKUU WA SERIKALI

Dkt. Beatrice Mutayoba
MKURUGENZI WA KINGA

Dkt. Khalid Massa
MKURUGENZI MSAIDIZI, SEHEMU YA AFYA MAZINGIRA NA USAFI

Bi. Catherine Sungura
AFISA HABARI MWANDAMIZI
WIZARA YA AFYA

### Msanifu

Bw. Said Nyaoza



Wizara ya Afya
S.L.P 743
**Dodoma, Tanzania**

Simu: +255-26-2323267/5
Rununu: +255-26-2342000/5
Barua pepe: ps@afya.go.tz

***www.moh.go.tz***
***wizara_afyatz***

# SUALA LA USAFI LIWE ENDELEVU - DKT. MPANGO



Mwanza

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Phillip Mpango amewataka wakuu wa Mikoa na Wilaya nchini kuhakikisha suala la usafi kwenye barabara kuu zinazounganisha Mikoa na Wilaya linakuwa endelevu.

Dkt. Mpango ameyasema hayo wakati akifungua Jukwaa la Nane la Maendeleo Endelevu jijini Mwanza lenye lengo la kujadili usimamizi madhubuti wa fukwe kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Pamoja na usafi wa mazingira, Dkt. Mpango anaagiza Mikoa na Halmashauri kuhakikisha wanaweka utaratibu wa kudhibiti utupaji taka hovyo barabarani baada ya watu kula vyakula au vinywaji wawapo safarini.

“Unapoangalia pembeni mwa barabara zote unaona zimegeuzwa jalala, mtu ukinywa maji chupa zinatupwa hovyo, makaratasi ya chakula yamejaa barabara zote, Taifa haliwezi kuendelea na utaratibu huu.”



Aidha, Dkt. Mpango pia anawasihi watendaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kulichukulia kwa umuhimu suala la uhifadhi wa mazingira ikiwemo kupanda miti na kuifuatilia kwa manufaa ya Taifa.

Tayari Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, imetoa maelekezo kwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) na wadau kuhakikisha barabara zinazounganisha mikoa na wilaya zinawekwa katika hali ya usafi.

Pia wizara hizo zimefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maelekezo iliyoyatoa ili kuhakikisha barabara kuu zinakuwa safi nyakati zote.

Aidha, kupitia shughuli za usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, usafi katika barabara kuu umeendelea kufanyika katika halmashauri zote kupitia Kitengo cha Udhibiti wa taka na usafi na kuhakikisha vyombo vya usafiri vina vifaa vya kutunzia taka ili kuepusha utupaji wa taka ovyo.






# TANZANIA BILA EBOLA NA MAGONJWA YA MLIPUKO INAWEZEKANA - WAZIRI UMMY

Kagera

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amesema ili kuhakikisha ugonjwa wa Ebola na magonjwa mengine ya mlipuko hayaingii nchini, kila mwananchi anatakiwa kuzingatia ipasavyo kanuni za afya.

Waziri Ummy anayasema hayo mkoani Kagera wakati wa kukagua utayari wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo Ebola.

Anasema ni vema kila mwananchi akazingatia kanuni za afya ikiwa pamoja na kuandaa vifaa kinga vya unawaji mikono katika makazi yao na maeneo ya kufanyia biashara.

Waziri Ummy anatumia fursa hiyo kuhamasisha namna ya kuchukua tahadhari na kujikinga na magonjwa ya mlipuko ikiwemo Ebola kwa wananchi waishio mipakani.

"Wananchi mnapaswa kuchukua hatua madhubuti kwa kunawa mikono mara kwa mara, watumishi chukueni hatua muhimu za kuwatambua wenye dalili, tukifanya hivi Tanzania itakuwa salama na magonjwa ya milipuko ikiwemo Ebola."

" Hivyo niwatoe hofu Watanzania kuhusu Ugonjwa wa Ebola uliopo nchi jirani, tunachopaswa kufanya ni kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga zinazotolewa na wataalam wa afya kama vile kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kutokugusana mikono na uonapo dalili nenda kituo cha kutolea huduma za afya."

Waziri Ummy anasisitiza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inafanya jitihada zote usiku na mchana kuhakikisha ugonjwa wa Ebola na magonjwa mengine ya mlipuko hayaingii nchini.

Pia anatumia fursa hiyo kukabidhi vifaa kinga na nyenzo za kutolea elimu kwa umma vilivyotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Management and Development for Health (MDH) ikiwemo vifaa vya kunawia mikono katika Soko la Kimataifa la Ndizi la Murongo mpakani mwa Tanzania na Uganda.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na vipima joto (thermoscanner), vitakasa mikono (sanitizers), barakoa, ndoo za kunawia mikono, vipaza sauti, mabango na vipeperushi kwa ajili ya kutolea elimu na uhamasishaji kwa jamii.

Katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Maji zinatekeleza mradi wa imarisha upatikanaji wa maji katika kituo cha afya cha Kabyaile ambacho kimetengwa kwa ajili ya kupokelea wahisiwa wa ugonjwa wa Ebola mkoani Kagera. Mradi huo unathamani ya shilingi milioni 200.





## TANZANIA YABUNI MFUMO WA KUMENG’ENYA TAKA ZA KIBAIOLOJIA KATIKA HOSPITALI

Dar es Salaam

TANZANIA imebuni mfumo wa mtambo wa kumeng’enya taka za kibaiolojia ambao unatumika katika Hospitali ya Mwananyamala na Sinza katika Jiji la Dar es Salaam.

Mtambo huo wa kumeng’enya taka na kuhifadhi salama kondo la nyuma pamoja na mabaki ya vyakula kutoka kwa wagonjwa na kuzalisha biogesi inayotumika kama nishati mbadala katika hospitali hizo tangu mwaka 2017.

Mbunifu wa mtambo huo kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Honest Anicetus anasema katika nchi zinazoendelea pamoja na Tanzania, uhifadhi salama wa taka zitokanazo na sehemu ya mwili wa binadamu kama vile kondo la nyuma baada ya mama kujifungua katika vituo vya kutolea huduma ya afya imekuwa changamoto.



“Mtambo wa kumeng’enya taka za kibiologia ni teknolojia inayofaa kutumika katika uhifadhi salama taka zinazotokana na huduma za afya, ambayo ni vigumu kuzihifadhi kwa salama kama vile kondo la nyuma kwa vile huharibika haraka na kuanza kutoa harufu muda mfupi baada ya mzazi kujifungua,” anasema Dkt. Honest.

Anasema mfumo huo una uwezo wa kuzalisha nishati ya biogesi ni matokeo ya bakteria wa methanojeniki kumeng’enya kwa kuvunjavunja kondo la nyuma. Nishati hiyo inayozalishwa hukidhi mahitaji ya kupikia, kuchemshia maji na kufulia katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha, Dkt. Honest anasema ili kuhakikisha ufanisi wa mtambo huo, unapaswa kusafishwa kwa kuchota tope (sludge) lililokaa chini kila baada ya miaka 5-8 kutegemea na matumizi.
“Lengo la kutoa tope zito ni kupata nafasi ya kupokea taka zingine kwa ajili ya kumeng’enywa, kwa kuwa tope hilo likiendelea kuwepo kwenye tangi hupunguza nafasi na kuathiri utendaji kazi wa mtambo huo.”

Anaelezea mitambo miwili ya umeng’enyaji taka za kibiolojia imejengwa chini ya ardhi na sakafu ya matangi yake imejengwa kwa zege huku kuta zake zikijengwa kwa matofali ya saruji na kusakafiwa isipenyeze maji.

“Mitambo hii ina uwezo wa mita za ujazo 32 kila moja, imeunganishwa na choo cha kisasa kilichopo kwenye jengo la wazazi ambacho kinaruhusu kusukuma kondo la nyuma linalotumbukizwa moja kwa moja katika mfumo wa umenge’nyaji.”

“Shughuli ya enzymatic ya bakteria kwa kiasi kikubwa inategemea joto, ambalo ni sababu muhimu kwa uzalishaji wa gesi ya methane kwa kuwa bakteria wa Methanojeni hawafanyi kazi vizuri katika halijoto ya juu ya nyuzi joto 50 au chini ya nyuzi joto 10,” anasema.

Metabolic mmenyuko huongezeka na kupungua kutegemeana na kiwango cha joto ndani yam tambo katika utengenezaji wa methane. Kiwango kizuri kwa umengenyaji kinapaswa kuwa nyuzi joto 28 hadi 40.

Uzalishaji wa gesi wa kuridhisha hufanyika katika safu ya mesophilic ambapo halijoto bora zaidi ni nyuzi joto 35 na katika hali ya hewa ya baridi, joto la vitu vya kuchachusha kwenye mmeng’enyo linahitaji kuongezeka hadi kufikia nyuzi joto 35.

Pia uzalishaji wa gesi unaweza kuongezwa kwa kiasi kikubwa kwa ongezeko la joto hadi nyuzi joto 55 na zaidi ya hapo uzalishaji huanguka kwa sababu ya uharibifu wa kimeng'enya cha bakteria kwa joto la juu. Kiwango cha uzalishaji gesi kinakadiriwa kuwa kati ya mita za ujazo 2.5- 5.0 kutegemeana na ukubwa wa mtambo na ufanisi katika ulishaji wa mtambo.





# TANZANIA YAJIDHATITI KUZUIA MLIPUKO WA EBOLA

Kagera

WIZARA ya Afya kupitia Idara ya Kinga, sehemu ya Afya Mipakani imejidhatiti kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola ili kuepusha ugonjwa huo kuingia nchini.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuimarisha uchunguzi wa awali ikiwemo kuwapima wasafiri wote wanaoingia na kutoka nchini kupitia mipaka yote rasmi.

Pia kuwapima wasafiri wa ndani ambao wanatembelea mikoa yenye hatari ya kupata mlipuko wa ugonjwa wa Ebola.
Mikoa ambayo iko kwenye hatari zaidi ya kupata ugonjwa wa Ebola nchini ni Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dar es Salaam.

Mkoa wa Kagera upo katika hatari kubwa zaidi kwa kuwa ina halmashauri saba zenye mipaka inayopakana na nchi zinazokumbwa mara kwa mara na ugonjwa huo.
Mipaka hiyo ni iliyopo Wilaya ya Ngara ikiwemo Rusumo ambao unapakana na nchi Rwanda, mipaka ya Murusagamba na Kabanga inapakana na nchi ya Burundi

Pia kuna mipaka sita inayopakana na Uganda ambayo ni Murongo Wilaya ya Kyerwa; Mutukula, Bugango, Minziro, Kashenye na Kakunyu iliyopo Wilaya ya Missenyi.

Katika kutekeleza hayo, Serikali imeendelea kuimarisha huduma ya kupima joto la mwili kwa wasafiri wote wanaoingia nchini kupitia mipaka yote ili kubaini wale watakaokuwa na zaidi ya nyuzi joto 37.5 ambalo ni miongoni mwa kiashiria cha kuambukizwa ugonjwa wa Ebola.

Umakini wa watumishi wa afya mipakani unasaidia wasafiri wote wanaotoka katika maeneo yenye maambukizi kuingizwa kwenye rejesta maalumu na orodha hiyo kuwasilishwa kwa timu ya ufuatiliaji ambapo kufikia Desemba 31, 2022 jumla ya wasafiri 19,542 wamefanyiwa uchunguzi na kufuatiliwa afya zao kwa muda wa siku 10 waliruhusiwa kuingia nchini.

Aidha, uchunguzi wa wasafiri kutoka nchini Uganda waishio umbali wa kilomita 10 za ujirani mwema katika mipaka ya Mutukula na Murongo na hadi kufikia Desemba 31, 2022 wasafiri wapatao 176,412 wamechunguzwa.

Mafanikio hayo yanatokana na juhudi za Serikali kuhamasisha wasafiri kutoa taarifa za afya zao kwa kutumia dodoso maalumu ili kubaini msafiri mwenye historia ya kutembelea nchi zenye maambukizi ya Ugonjwa wa Ebola katika kipindi cha siku 21, msafiri aliyekuwa karibu na mgonjwa ama aliishi naye, kushiriki mazishi au kumhudumia.

Timu ya viongozi kutoka Wizara ya Afya wakiongozwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu ambaye aliambatana na wataalamu kutoka Idara ya Kinga, Kitengo cha Afya, Mazingira na Usafi pamoja na Elimu ya Afya kwa Umma walitembea Mkoa wa Kagera hususani kwenye mipaka ya Kashenye, Wilaya ya Missenyi na mpaka wa Murongo Wilaya ya Kyerwa na kuwahamasisha wananchi kuendelea kuchuka tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Aidha, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi alitembelea mipaka ya Minziro na Mutukula wilayani Missenyi na kuhimiza uzingatiwaji wa mikakati ya kukabiliana na ugonjwa wa Ebola usiingie nchini.

Mwingiliano wa wananchi wanaoishi Uganda na Tanzania ni mkubwa kupitia mipaka isiyo rasmi zaidi ya 1,200 kwa Mkoa wa Kagera na mipaka isiyo rasmi takribani 435 ya Uganda ambayo wananchi wa nchi zote mbili huchangamana kutokana na shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo huduma za shule, zahanati na maeneo ya biashara.

Kutokana na muingiliano huo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dkt. Issessanda Kaniki aliongoza timu ya Tanzania kwa kufanya mkutano baina ya Tanzania na Uganda ili kuhimiza kila upande kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti ugonjwa wa Ebola kwa wananchi ili kulinda afya zao.



# PROGRAMU YA SRWSS YAFANYA VIZURI VIASHIRIA VYA AFYA, MAJI, ELIMU



Dodoma

UTEKELEZAJI wa Programu ya Huduma Endelevu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (SRWSS) umefanya vizuri katika viashiria vyote vya mradi vya maji, afya na elimu.

Mradi huu ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2019/2020 unatekelezwa katika halmashauri 86 za mikoa 17 kwa gharama ya shilingi trilioni 1.5 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Haya yameelezwa na Mratibu wa Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira kutoka Wizara ya Afya, Anyitike Mwakitalima wakati wa kuelezea hali ya utekelezaji na ufikiaji wa shabaha katika mradi huo.

Mwakitalima anasema awamu ya kwanza ililenga kuwezesha upatikanaji wa maji kwa watu milioni 3, uboreshaji wa vyanzo vya maji katika vijiji 45,000, upatikanaji wa vyoo bora ngazi ya jamii kwa watu milioni 4.

Pia kuondoa tabia ya kujisaidia hovyo katika vijiji 1,250, kuboresha miundombinu ya maji na usafi katika vituo vya afya 1,500, shule za msingi 1,500 kwa kipindi cha miaka mitano.

Mwakitalima anasema mafanikio yaliyopatikana kwenye mradi huo ni kuongezeka kwa kaya zenye huduma za vyoo bora hadi kufikia kaya 7,060,420 Septemba, 2022 kutoka 6,102,552 Desemba, 2019 hivyo kuzidi lengo lililotarajiwa la kufikia kaya 4,000,000.
Anasema pia vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 1,536 vimeboresha miundombinu ya maji na usafi wa mazingira ikiwa ni zaidi ya vituo 1,500 vilivyotarajiwa.



Aidha, Mwakitalima anasema shule za msingi zipatazo 2,398 ikiwa ni zaidi ya 1,500 zilizolengwa zimeboreshewa miundombinu ya maji, vyoo na vifaa vya kunawia mikono, huku vijiji vilivyoacha tabia ya kujisaidia hovyo vimefikia 4,794 ikiwa ni ongezeko la vijiji 900 kutoka vijiji 3,894 kwa kipindi hicho.

Watekelezaji wa mradi huo ni Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Mradi unalenga kuboresha huduma za maji safi na salama na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini kwenye mikoa na halmashauri zinazotekeleza mradi huo.

Wizara ya Afya ina kazi ya kuratibu usafi ngazi ya kaya na huduma za maji na usafi katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyoo bora vinavyozingatia mahitaji maalumu na vifaa vya kunawia mikono ngazi ya kaya na vituo vya kutolea huduma za afya, ujenzi wa miundombinu ya maji, ukarabati wa jengo la kujifungulia wazazi kwa kuweka miundombinu ya maji na bafu na udhibiti wa taka.

Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inawajibika kuhakikisha majisafi na salama yanapatikana kwenye maeneo yote ya mradi hususani maeneo ya vijijini.

Kwa upande wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inawajibika kusimamia usafi katika shule za msingi kwenye maeneo ya mradi wakati Ofisi ya Rais-TAMISEMI wanasimamia utekelezaji wa mradi katika Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Awamu ya kwanza ya mradi ilianza kwa halmashauri 86 ndani ya Mikoa 17 ya Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Geita, Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Rukwa, Songwe, Iringa, Manyara, Ruvuma, Lindi na Mtwara ambayo ilipatikana kwa kigezo cha hali duni ya upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira, kiwango cha umasikini na udumavu wa watoto.

Mwakitalima anasema fedha za kuendesha programu hii hutolewa kulingana na matokeo ambayo yanapatikana kwa mfumo wa lipa kwa matokeo (PforR) huku asilimia 10 ya fedha hizo huelekezwa katika utekelezaji wa shughuli za usafi ngazi ya kaya.

Kutokana na mafanikio hayo, Benki ya Dunia imeongeza wigo wa mkopo kwa awamu ya pili wa shilingi bilioni 690 itakayoanza mwaka 2023 hadi 2025 ikiongezeka mikoa nane ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Njombe, Morogoro, Pwani, Dodoma na Mbeya. Hivyo kufanya programu hiyo kutekelezwa katika mikoa 25 na halmashauri 137.

# UZINGATIAJI KANUNI ZA AFYA NI KINGA DHIDI YA MARADHI

Dodoma

UKAGUZI wa maeneo ya makazi, biashara au ofisi ni shughuli muhimu katika uzingatiaji wa kanuni bora za afya nchini.


Kwa kuzingatia hilo, Kitengo cha Huduma za Afya Mazingira cha Wizara ya Afya kimeendelea kusimamia eneo la huduma ambalo kimsingi linasaidia katika uondoshaji na udhibiti wa machukizo (Nuisance) ambayo huchangia kueneza magonjwa ya kuambukiza na yasioambukiza.

Katika kipindi cha Julai-Desemba, 2022, maeneo mbalimbali yamekaguliwa na halmashauri na hatua stahiki kuchukuliwa kulingana na hali iliyobainika.

Maeneo yaliokaguliwa ni pamoja na kaya, shule, nyumba za ibada, masoko, hoteli, nyumba za kulala wageni, sehemu za kuuzia vyakula, maeneo ya burudani, ofisi za umma, vyuo na mabenki.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa kaya zilikuwa na idadi ndogo zaidi asilimia 50 ya vifaa vya kunawia mikono.

Maeneo mengine yanaoneshwa katika mchoro






Ukaguzi huo huambatana na utozwaji wa faini za papo kwa papo kwa maeneo yanayobainika kutokidhi vigezo vya usafi na afya. Jumla ya ilani 14,528 zilitolewa na shilingi 88,620,164 zilikusanywa ikiwa ni faini za papo kwa papo.

Kuhusu changamoto za utekelezaji shughuli za usafi, tathimini inaonesha kuwa maeneo yanayokaguliwa yamebainika kutokuwa na vifaa vya kunawia mikono, mwamko mdogo wa baadhi ya wananchi na viongozi katika shughuli za usafi kwani hawajitokezi katika kutekeleza shughuli za usafi katika maeneo yao.

Pia uwepo wa wingi wa chupa za vinywaji, nepi za watoto (diapers) na vifungashio katika madampo, utupaji taka hovyo hasa katika njia kuu za usafiri na makazi ya watu, rasilimali kidogo zinatengwa kwa ajili ya shughuli za udhibiti wa taka.

Changamoto nyingine ni taka kutoondoshwa kwa wakati katika mitaa kutokana na ukosefu wa wazabuni au vikundi vyenye nyezo za uhakika na uhaba wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya uondoshaji wa taka.

Kuhusu fursa zilizopo katika udhibiti wa taka, tathimini inaonesha kuna mwamko mzuri wa wananchi katika udhibiti wa taka na uwepo wa viongozi wa mfano katika kuhamasisha huduma za uondoaji taka.

Vile vile, uwepo wa kampuni ya usafi yenye uwezo wa kutekeleza shughuli za usafi katika majiji na manispaa na miji nchini na uwepo wa vikundi vya kijamii na sekta binafsi kwenye utoaji wa huduma za afya mazingira na usafi.


Katika kuboresha huduma za afya mazingira na usafi hususani udhibiti wa taka, Kitengo kimeandaa utaratibu wa ufuatiliaji wa karibu wa kila siku kwa maeneo yote ya mijini na kupitia Kundi Sogozi la WhatsApp hatua ambayo imerahisisha mawasiliano ya haraka na wasimamizi wa usafi pindi zinapopokelewa kero ya uwepo wa uchafu kutoka kwa wananchi.

Aidha, kwa maeneo yenye changamoto kubwa kitengo kimepanga utaratibu wa kutembelea maeneo husika na kujadiliana namna bora ya kuzishughulikia changamoto zinazozorotesha utoaji wa huduma.
Kazi ya ufuatiliaji wa moja kwa moja kwenye mikoa na halmashauri imeshaufanyika katika mikoa ya Singida na Dodoma. Mipango iliyopo ni kutembelea mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara, Iringa, Mbeya na Songwe.

# HABARI PICHA

















# SONGWE WAIMARISHA AFUA ZA UNAWAJI MIKONO, USALAMA WA MAJI YA KUNYWA

WIZARA ya Afya kwa kushirikiana na wizara za kisekta, wadau, mikoa na halmashauri zinafanya kazi kubwa ya kuhamasisha jamii ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya umma kuzingatia usafi na kudumisha usafi wa mazingira.

Hatua hiyo inalenga kuimarisha udhibiti wa magonjwa yatokanayo na uchafu kama vile kipindupindu, homa ya matumbo na UVIKO-19.

Pamoja na juhudi hizo, jamii ya watanzania hususani wale wa vijijini wamekuwa na changamoto ya kuwa na vifaa sahihi na bora vya usafi ikiwemo vifaa vya kunawia mikono na utunzaji salama wa maji ya kunywa. Katika kufikia azma hii, Mkoa wa Songwe umekuja na ubunifu na kuanzisha kampeni ya kuwezesha kaya kupata ndoo zenye koki kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa au unawaji mikono.

Katika kufikia azma hii, Mkoa wa Songwe umekuja na ubunifu na kuanzisha kampeni ya kuwezesha kaya kupata ndoo zenye koki kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa au unawaji mikono.

Hivyo, mkoa umeweza kununua koki za maji na vifaa vya kutobolea ndoo ili kutoa huduma ya kufungaji wa koki kwenye ndoo za wanakijiji.

Kwa huduma hiyo, mwananchi wanatakiwa kuwasilisha ndoo katika ofisi ya kijiji ambapo wataalamu kutoka ngazi ya Halmashauri ambao wanafika kwa ajili ya kutoa elimu ya usafi hufunga koki kwenye ndoo hizo kwa gharama nafuu.

Kupata huduma hiyo, wananchi huchangia Sh 3,000 kwa kazi hiyo ambayo ikilinganishwa na gharama ya kununua ndoo ndogo yenye koki inayouzwa zaidi ya Sh 20,000 madukani.
Katika ziara ya kushuhudia mafanikio ya utekelezaji wa Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Afya Mazingira na Usafi, Dkt. Khalid Massa anakagua miundombinu ya Maji, vyoo na vifaa vya kunawia mikono katika vituo vya kutolea huduma za afya na kushiriki kutoboa ndoo 29 za wananchi tayari kwa kufugiwa koki.

Akiwa katika Kijiji cha Mbozi kilichopo Kata ya Igamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, Dk Massa anashiriki katika kuhamasisha suala la usafi kwa kugawa sabuni za maji kwa ajili ya kunawia mikono.

Pia anashiriki katika kutoa elimu ya umuhimu wa utunzaji salama wa maji ya kunywa pamoja na unawaji mikono kwa maji tiririka na sabuni kwa wananchi waliofika kupata huduma.

Aidha, Dkt. Khalid Massa alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa halmashauri zingine za Mkoa wa Songwe na mikoa mingine kuendelea kutekeleza afua za usafi wa mazingira.

“Ni vyema kuja na ubunifu wa kuboresha utoaji wa huduma hizo ili kuwezesha jamii kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Akizungumzia kampeni inayolenga kuhakikisha kila kaya inakuwa na chombo sahihi kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa na kunawa mikono, Afisa Afya Mkoa wa Songwe, George Mgallah anasema afua hii ni muhimu katika suala zima la usafi.

“Ni afua muhimu kwa sababu itawawezesha wananchi kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni na hivyo kuondoa hatari ya kusambaa kwa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya uchafu.”

Anasema pia wananchi wataweza kutunza vizuri maji ya kunywa yaliyochemshwa au kutibiwa kwa njia ya vidonge, kutunza maji ya kunywa katika ndoo safi zenye koki na mfuniko hivyo kujikinga na magonjwa yanayoweza kuenezwa kwa kunywa maji yasiyo salama.

Naye, Mratibu wa kampeni hiyo, Emmanuel Martine anasema kumekuwa na mwitikio mkubwa wa wananchi kujitokeza kufungiwa koki katika kampeni ambayo mpaka sasa imefanyika katika Halmashauri ya Mbozi, Ileje na Momba huku Halmashauri za Songwe na Tunduma zikiwa mbioni kufikiwa.

“Pia wataalamu wanaendelea kuhamasisha jamii husika kuzingatia kanuni za afya na usafi ikiwemo usalama wa maji ya kunywa na unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni kwa nyakati zote muhimu.”

Anasema Mkoa wa Songwe unaendelea na taratibu za kuendelea kuzifikia kaya za halmashauri zote za mkoa ili waweze kutekeleza kampeni hii.




# VYOO BORA VIMEONGEZEKA TANZANIA

Dodoma

UWEPO wa vyoo bora umeongezeka hapa nchini katika ngazi ya kaya hadi kufikia asilimia 72.6 mwaka 2022 kutoka asilimia 19.5 kwa mwaka 2012.

Kwa upande wa kaya zisizokuwa na vyoo zimepungua kutoka asilimia 20.5 hadi kufikia asilimia 1.4, huku ikidaiwa kuwa mtu mmoja ambaye hana choo hupoteza takribani saa 58 kwa mwaka kutafuta mahali pa kujisitiri.

Hayo yameelezwa jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Matumizi ya Choo Duniani ambayo hufanyika mwezi Novemba kila mwaka.

"Ujenzi wa vyoo bora pamoja na uwepo wa huduma za majisafi na salama umeongezeka katika taasisi zetu, mfano shule za msingi na vituo vya kutolea huduma za afya, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita takribani shule za msingi 2,500 zimejengewa vyoo bora," anasema Dkt. Shekalaghe.

Anasema kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 1,500 vimeboreshewa huduma ya maji, vyoo na sehemu za kunawa mikono. Sambamba na uboreshwaji wa huduma ya vyoo katika kaya na taasisi, eneo la usafi katika njia kuu nalo limeboreshwa kwa kiasi kikubwa.

"Ufuatiliaji uliofanywa na wizara mwaka jana umeonesha kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zaidi ya vituo vya njiani vya mabasi 280 vimejengwa na Serikali pamoja na sekta binafsi ambapo huduma ya vyoo bora inapatikana wakati wa safari," anafafanua Dkt. Shekalaghe.

Anataja maeneo yaliyojengwa vyoo kuwa ni maeneo ya mizani, vituo vya kuuzia mafuta, hoteli na migahawa na kuwa vyoo hivyo vimesaidia kupunguza tatizo la kujisaidia hovyo wakati wa safari maarufu kama kuchimba dawa.

Anasema kuwa Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa huduma bora katika vituo na kuhamasisha uwekezaji hususani kupitia sekta binafsi ili maeneo mengi zaidi yaweze kutoa huduma kwa wasafiri na wasafirishaji katika kiwango cha ubora.

Ujenzi wa vyoo bora unaambatana na uwekaji wa vifaa vya kunawia mikono katika kaya, maeneo ya biashara na taasisi.

Tathmini iliyofanywa na Wizara ya Afya, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kunawa Mikono Duniani Oktoba 15 iliyokuwa na kauli mbiu 'Tuungane kuhakikisha usafi wa mikono kwa wote', imeonyesha kuna ongezeko la kaya zenye vifaa vya kunawia mikono kutoka asilimia 21 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 47.6 Juni, 2022.

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inaendelea kuhimiza kila kaya, maeneo ya biashara na taasisi waweke vifaa vya kunawia mikono na kuvitumia kabla ya kula, kabla ya kutayarisha chakula, baada ya kutoka chooni, kabla ya kutayarisha chakula cha mtoto, kabla ya kumlisha mtoto na baada ya kumtawaza mtoto.

Shirika la Afya duniani, kupitia tafiti linaeleza unawaji wa mikono unapunguza magonjwa ya kuambukiza kwa zaidi ya asilimia 50.





# UTARATIBU WA KUNAWA MIKONO UWE ENDELEVU – PROF. NAGU


Kagera

MGANGA Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu amewaagiza Maafisa Afya wa mikoa yote nchini ikiwemo Mkoa wa Kagera kuweka utaratibu endelevu wa wananchi kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.

Hatua hiyo ni katika kujikinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko kama vile Ebola na magonjwa yanayoenezwa na vimelea vya uchafu.

Prof. Nagu anayasema hayo akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Kagera alipotembelea Kituo cha Afya cha Kabyaile kilichopo Wilaya ya Missenyi kinacho wahudumia wahisiwa wa Ugonjwa wa Ebola.

Anasema wajibu wa Maafisa Afya ni kuwakumbusha wananchi juu ya usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi na kusisitiza kuwa kutofanya usafi wa mazingira ndio sababu kuu ya maradhi.




Aidha, Profesa Nagu anatumia fursa hiyo kuwasihi wananchi kudumisha ratiba ya usafi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa taka ngumu na maji machafu.

"Uboreshaji wa mazingira una manufaa makubwa kwa afya ya kila mtu katika kaya na jamii nzima, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha mazingira yanayomzunguka yanakuwa safi," anasisitiza Prof. Nagu.

Anasema kuwa udhibiti wa majitaka na kinyesi ni muhimu kwa sababu utasaidia kuepusha maambukizi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Prof. Nagu anawasisitiza Maafisa Afya kuendelea kuwajengea wananchi uelewa juu ya magonjwa ya mlipuko yanayoweza kueneza magonjwa yatokanayo na uchafu.




# UNICEF, SNV YASHIRIKI KUIMARISHA AFYA YA WATANZANIA

Shinyanga

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inawahudumia wananchi katika maeneo mbalimbali ya kutoa huduma kwa jamii ikiwemo vyoo bora ili kuwahakikishia afya njema na ustawi wa watu wa rika zote nchini.

Kwenye sekta ya afya, ushirikiano huo umedhihirishwa kwa kujenga vyoo bora katika maeneo ya kutoa huduma za kijamii ikiwemo shule, vituo vya mabasi na hospitali ili kuondoa ukosefu wa huduma hizo katika maeneo ya kazi na makazi ya watu.

Katika Manispaa ya Shinyanga ushirikiano wa wadau na Serikali umejidhihirisha kwa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kusaidia ujenzi wa vyoo bora vya kisasa katika kituo kikuu cha mabasi kilichogharimu shilingi milioni 130 na vinatumika kutoa huduma kwa wasafiri kwa kuzingatia mahitaji maalum kwa watoto, wanawake na walemavu.

Pia vyoo hivyo vimechangia Manispaa ya Shinyanga kuwa mshindi wa kwanza katika Shindano ya Afya na Usafi wa Mazingira mwaka 2022 katika kundi la manispaa na kuwa kinara wa shughuli za usafi kwa kundi la manispaa kutokana na azma ya viongozi wa mkoa huo pamoja na watalaam kusimamia suala la usafi.

Vile vile vyoo hivyo ni chanzo adhimu cha mapato na kinaingizia halmashauri hiyo kiasi cha shilingi 800,000 kwa siku.

Aidha, kimekuwa ni chanzo cha nishati inayotumika kwenye mgahawa uliopo eneo hilo ambao unatumia gesi inayozalishwa kutokana na tope kinyesi kinachozalishwa katika vyoo hivyo.

Pia maji yanayozalishwa kwenye vyoo hivyo hutibiwa na kutumika kumwagilia majani ikiwa ni njia mojawapo ya kuweka safi mazingira ya manispaa hiyo.

Kwenye sekta ya elimu, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) limetoa mchango wa kujenga vyoo vya kisasa katika Shule ya Msingi Mtumba iliyopo kata ya Mtumba Halmashauri ya Jiji la Dodoma vyenye thamani ya shilingi milioni 161.

Mkurugenzi wa Kinga Wizara ya Afya, Dkt. Beatrice Mutayoba amewasihi viongozi na walimu wa shule hiyo kulinda na kutunza miundombinu ya maji na vyoo viliyojengwa shuleni hapo ili kutoa huduma iliyokusudiwa. "Tafiti zinaonesha kuwa, shule zenye miundombinu bora ya maji na usafi wa mazingira huchangia wanafunzi kutumia muda mrefu zaidi shuleni ikilinganishwa na shule ambazo hazina miundombinu, hivyo kuchagiza wanafunzi kufanya vizuri."

"Vyoo hivi vimezingatia mahitaji ya makundi yote wakiwemo watumishi, wanafunzi wakike na wa kiume na wenye ulemavu, pia kuna miundombinu ya unawaji wa mikono kwa pamoja bila kusahau uwepo wa kiteketezi kwa ajili ya kuchomea taulo za kike zilizotumika."





# HEDHI SALAMA, UTU WA MWANAMKE

Kigoma

JUHUDI za Serikali, mashirika ya kijamii na watu binafsi ni kumsitiri mtoto wa kike na mwanamke wakati wa hedhi.

Katika kutekeleza hilo, Wizara ya Afya ipo mstari wa mbele kuhamasisha jamii kutambua na kuthamini suala la hedhi salama kwa afya bora ya wasichana na wanawake nchini.

Hata hivyo, upatikanaji wa taarifa na vifaa kwa mtoto wa kike na mwanamke wakati wa hedhi ni jambo linalochagizwa na mazingira wezeshi wakati wa hedhi, ili wawe huru kutekeleza majukumu kikamilifu na kutoa mchango katika kujenga uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

Katika kuthamini suala hilo, kila ifikapo Mei 28 kila mwaka, Tanzania huungana na mataifa mengine duniani na wadau wa Afya ya Hedhi na Usafi kuadhimisha Siku ya Hedhi Salama ili kujenga uelewa kwa kila mwanamke.

Hatua hiyo inamsidia mtoto wa kike na mwanamke kusimamia hedhi yake kwa njia ya usafi popote alipo, kwa faragha, usalama na kwa heshima.

Kwa mwaka 2022, maadhimisho ya Hedhi Salama yalifanyika mkoani Kigoma huku Mgeni rasmi akiwa ni Mwenza wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa - Mbonimpaye Mpango ambaye alitumia fursa hiyo kuhamasisha watanzania kushiriki na kufanikisha ajenda ya hedhi salama nchini.







“Ni wajibu wa kila mtu, viongozi wa Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali pamoja na jamii kutambua kuwa hedhi salama ni muhimu kwa afya, maendeleo na utu wa mwanamke na mtoto wa kike ambaye yuko shule za msingi, sekondari, vyuo na wale waliopo nyumbani kuwa wote wanahitaji kupata mahitaji hayo bila kuwa na kizuizi chochote.”

Anasema wakati umefika kwa kila mtu kuvunja ukimya na kupaza sauti juu ya suala la hedhi salama na kujikita zaidi kuboresha upatikanaji wa bidhaa za hedhi zenye bei nafuu na vifaa rafiki ili kuwasaidia wanawake na wasichana wote nchini.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi anasema ifikapo mwaka 2030 inatarajiwa kuwe na ulimwengu ambao hakuna mwanamke au msichana atakayeachwa nyuma katika sekta yeyote kisa tu anapata changamoto ya kumudu gharama za taulo za kike, kupata maji salama na vyoo bora ambavyo huchangia kudhoofisha fursa ya elimu, afya na hali ya kijamii kwa wanawake na wasichana duniani kote.

Anasema mikakati iliyopo sasa katika kuboresha eneo la hedhi salama, ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Kitaifa na zana zake.





# SERIKALI YADHIBITI TAKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Dodoma

SERIKALI inasimamia udhibiti salama wa taka zinazotokana na huduma za afya ili kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa wafanyakazi wa sekta ya afya, kulinda afya ya umma na mazingira katika vituo vya kutolea huduma za afya Tanzania Bara.

Licha ya taka zinazozalishwa kutokana na huduma za afya bado ni changamoto kubwa katika kuboresha huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma ya afya nchini, Serikali inaendelea kupunguza uchafuzi wa hewa na kuenea kwa magonjwa yanayosababishwa na huduma duni za udhibiti taka hatarishi kwa kujenga vichomea taka katika hospitali, vituo vya afya pamoja na zahanati.

Tathimini ambayo imefanywa na Wizara ya Afya inaonesha usimamizi na udhibiti taka hizo umefanyika kwa kukagua maeneo na wafanyakazi wa hospitali za mikoa na wilaya kwa kuwatembelea na kujionea namna wanavyotekeleza majukumu yao ya kila siku katika maeneo yao ya kazi.

Ufuatiliaji huo umebaini kuwa utaratibu wa kutumia vifaa maalumu vyenye rangi za - utambulisho vya kutenganisha taka zinazotokana na huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya umeongezeka katika mikoa iliyofanyiwa ufuatiliaji.

Mikoa ambayo imefanya vizuri katika tathmini hiyo kwa zaidi ya asilimia 80 ni Geita 97.7, Mtwara 95.5, Tanga 94.5, Arusha 93.1, Kigoma 92.9, Songwe 92.5 na asilimia 90.3 katika Mkoa wa Njombe huku mikoa ambayo haijakufanya vizuri katika tathmini hiyo ambayo ipo chini ya asilimia 50 ni Ruvuma 48.2, Simiyu 40.4, Shinyanga 40.3 na Mkoa wa Pwani ambao una asilimia 35.4.

Aidha, kwa upande wa matumizi ya mifuko maalumu ya rangi kwa ajili ya kutenganisha taka hatarishi kimkoa, mikoa ya Tanga asilimia 92.1, Arusha 90.7, Geita 90.1 na Kigoma 89.0 imefanya vizuri katika tathmini kwa zaidi ya asilimia 80 wakati mikoa ya Mbeya 48.9, Rukwa 47.1, Simiyu 40.4 Shinyanga 35.2, Pwani 30.7, Ruvuma 23.3 na Mkoa wa Lindi asilimia 12.9 haijakufanya vizuri chini ya asilimia 50.

Katika kukabiliana na adha ya kuteketeza taka, Wizara ya Afya imekuja na mwarobaini wake kwa kujenga vichomea taka katika hospitali (High tech Incinerator) na katika vituo vya afya na zahanati kwa gharama nafuu (Demontfort Incinerator-Low cost).

Kwa upande wa hospitali, vichomea taka hivyo hujengwa kwa kutumia vifaa maalumu vya kuzalisha joto na vyenye uwezo mkubwa wa kuhimili joto la nyuzi joto 1,300 mpaka 1,600 ambavyo huendeshwa kwa kutumia umeme na vimejengwa kwenye hospitali za mikoa kwa asilimia 90 na wilaya asilimia 20.

Vichomea taka vilivyojengwa katika hospitali vina uwezo wa kutunza nyuzi joto 850 mpaka 950 kwa muda wote wa kutumika na kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi ya saa nane kwa siku.

Pia vina uwezo wa kuteketeza taka zenye uzito wa kilogramu 100 kwa saa, kuteketeza taka nyingi kutegemeana na ukubwa wake, ni rafiki kwa mazingira yenye uzalishaji mdogo wa gesi sumu na ni rahisi na rafiki kwa mtumiaji.

Kwa upande wa vituo vya afya na zahanati, vichomea taka vyake hujengwa kwa vifaa maalumu vya kujengea vyumba vya ndani na havitumii umeme, wala mafuta na vinauwezo wa kuingiza hewa ndani kupitia madirisha madogo yaliyopo pembeni na kuiacha iendelee kutumika kwa muda mrefu, hatua inayozifanya kuta za ndani kutengeneza joto jingi kwa muda mfupi.

Vichomea taka hivyo vinauwezo wa kufikisha nyuzi joto 850 mpaka 1,100 iwapo vitakuwa na taka kavu, taka zenye majimaji zikiwa nyingi hushusha joto mpaka nyuzi joto 500 na kuanza kutoa moshi mwingi na kusababisha uchafuzi wa mazingira. Aina hii ni rafiki kwenye vituo vya afya na zahanati tu.

Aina hiyo ya viteketezi taka vinavyojengwa katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya inafaida nyingi hasa gharama ndogo za ujenzi na uendeshaji, inadumu kwa muda mrefu ikitumiwa vizuri, ina uwezo wa kuteketeza taka nyingi kwa mara moja kwa zaidi ya kilogramu 40-50 kwa saa na ni rahisi kuzitengeneza na kuzikarabati.




# WATUMISHI 1,038 SEKTA YA AFYA WAPATA MAFUNZO USALAMA MAHALA PA KAZI

Dodoma

WATUMISHI 1,038 wa sekta ya afya kutoka vituo vya kutolea huduma za afya kwenye mikoa 10 nchini wamepata mafunzo ya uimarishaji wa mazingira ya afya kazini.

Mafunzo hayo yametolewa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia Kitengo cha afya Mazingira na Usafi cha wizara hiyo kati ya mwaka 2021 na 2022.

Mafunzo hayo yamelenga kuwezesha vituo vya kutolea huduma za afya, wafanyakazi na menejimenti za vituo kuwa na mjadala wa pamoja wa kuimarisha mazingira ya kazi ili kuzuia magonjwa, ajali na athari za kazi kwa watumishi wa sekta ya afya nchini.

Aidha, katika kufanikisha mafunzo hayo, wawezeshaji kutoka Wizara ya Afya walizisaidia hospitali za mikoa na halmashauri kuandaa mipango ya uimarishaji wa mazingira ya kazi kwa njia shirikishi.

Pia, kusaidia manejementi za hospital kuimarisha mazingira ya kazi ili kuhimili magonjwa, ajali na athari zitokanazo na kazi na kujenga uwezo wa kutatua changamoto kwa njia shirikishi kama hatua za kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi. Vilevile watumishi walipata mafunzo ya aina mbalimbali za athari namna ya kujikinga athari hizo kwa kushirikiana na menejementi.

Hata hivyo, tathmini katika mafunzo hayo imeonesha kuna haja ya kuongeza nguvu katika kuwezesha vituo vya kutolea huduma ikiwemo kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi katika maeneo ya matumizi ya muda wa kazi, muda wa kujishughulisha na shughuli nje ya kazi na namna ya kukabiliana na unyanyapaa, vurugu kutoka kwa wagonjwa au ndugu wa wagonjwa.

Pia uwepo wa vifaa saidizi ili kupunguza athari za kiigonomiki, kulinda afya, kupunguza ajali na maumivu ya kazi kwa watumishi ikiwemo kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji ili kuweka mazingira salama kwa wafanyakazi.

Mafunzo haya yalitolewa katika Hospitali 10 za Rufaa za Mikoa na hospitali za halmashauri za Wilaya 73 kutoka kwenye mikoa hiyo.

Hospitali hizo za rufaa ni Iringa, Kitete-Tabora, Mawenzi-Kilimanjaro, Mbeya, Maweni-Kigoma, Dodoma, Songea-Ruvuma, Sekou Toure-Mwanza, Ligula-Mtwara na Singida.






# MWONGOZO HUDUMA ZA MAJITAKA KWA JAMII KUANDALIWA

Dodoma

WIZARA ya Afya inaandaa mwongozo wa kitaifa wa utoaji bora na salama wa huduma za majitaka kwa jamii.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Afya Kazini kutoka Wizara ya Afya, Joseph Birago amesema mwongozo huo utazingatia afya na usalama wa watoa huduma, kuhifadhi usafi wa mazingira na kuziwezesha halmashauri namna bora ya kuratibu na kusajili watoa huduma za usafi wa mazingira.

"Mwongozo huu pia utawahusu watoa huduma binafsi na wanaoshirikiana kwa madhumuni ya kuboresha afya na usalama wa wafanyakazi,"anasema.

Anasema kuwa kuandaliwa kwa mwongozo huo kunatokana na tathmini iliyofanywa na wizara hiyo kwenye huduma za majitaka kwa kuangalia mazingira ya wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi ili kuangalia afya na usalama wa mazingira mahali pa kazi.





Birago anasema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Water AID Tanzania ilifanya tathmini na kubaini baadhi ya changamoto katika miji hususani maeneo yasiyopimwa ambayo hutegemea huduma za uondoshaji wa majitaka kwa watoa huduma wasio rasmi katika Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Arusha.

"Tulipofanya hii tathmini tuligundua wafanyakazi wengi wa sekta isiyo rasmi wanachangamoto kubwa kama vifaa duni vya maeneo yao wanayofanyia kazi, vifaa kinga, kutotambuliwa, na changamoto ya miundombinu ya mahali pa kwenda kutupa topekinyesi na ndio maana tukaona umuhimu wa kuja na mwongozo,"anasema.



## USAFI WA MAZINGIRA KUPUNGUZA MAGONJWA YA MLIPUKO KWA 70%

Dodoma

USAFI binafsi na usafi wa mazingira unaweza kupunguza magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafu kwa asilimia 70.

Hayo yameelezwa na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga, Dkt. Beatrice Mutayoba alipofanya usafi kwenye Soko la Bonanza lililopo Kata ya Chamwino jijini Dodoma wakati akizindua Wiki ya Usafi wa Mazingira na Matumizi ya Choo Duniani yanayofanyika Novemba 15-19 kila mwaka.

“Usafi wa mazingira unasaidia kupunguza asilimia 70 ya magonjwa ya mlipuko kama Kipindupindu, hivyo maofisa afya na watendaji wa kata mnapaswa kusimamia vizuri usafi wa mazingira mita tano kuzunguka maeneo ya nyumba zenu, ofisi, taasisi na maeneo ya biashara ili kuepuka magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na uchafu," anasema Dkt. Mutayoba.

Anasema kuwa kufanya usafi kwenye mazingira ya kuishi ni jambo jema na kunasaidia kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji chini ya ardhi na kudhibiti magonjwa ya mlipuko ikiwemo Kipindupindu na magonjwa mengine yanayosababishwa na uchafu.

“Ni vema kuweka usimamizi wa usafi na kusafisha mitaro ya maji ya mvua kwenye maeneo ya soko ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kama Kipundupindu.”

Katika kuhakikisha magonjwa ya mlipuko yanatokomezwa mkoani Dodoma, Mkuu wa Mkoa huo Rosemary Senyamule anatoa agizo kwa Maafisa Afya na Mazingira kusimamia usafi wa mazingira ili kuepuka magonjwa ya mlipuko katika kipindi cha mvua.







# USAFI WA KILA JUMAMOSI ULIVYO DHIBITI TAKA NGUMU

Dodoma

TATHIMINI inaonesha kuwa utekelezaji wa usafi wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, umesaidia kudhibiti taka ngumu nchini.

Hatua hiyo imetokana na Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kuitikia utekelezaji wa agizo la kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi ili kuimarisha usafi wa mazingira kwenye maeneo yao kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 iliyotoa tangazo la siku ya usafi, Mwaka 2016.

Katika tathimini ya hali ya udhibiti wa taka hizo kwa kipindi cha robo ya mwaka (Oktoba hadi Desemba, 2022) inabainisha namna halmashauri zinaendelea kutekeleza afua za udhibiti wa taka ngumu kwa kuhakikisha taka zinazozalishwa zinafikishwa katika madampo.

Miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa ili kuboresha huduma za udhibiti wa taka ngumu ni usafi wa mazingira wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi na ushiriki wa viongozi katika udhibiti uchafuzi wa mazingira.


Pia tathmini hiyo inaeleza kuwa katika Halmashauri 87 tani 195,112.42 za taka ngumu -




ngumu zilizalishwa, kati ya hizo tani 121,967.8 zilikusanywa na kupelekwa dampo sawa na asilimia 63 ya taka zote zilizozalishwa.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ni moja ya viongozi ambao wamekuwa wakisimamia kwa ukamilifu suala la usafi wa mazingira kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi ili kudhibiti taka na kuimarisha usafi wa mazingira.

Kadhalika, kwa Jiji la Dodoma, Mkurugenzi wake, Joseph Mafuru katika maeneo mbalimbali aliyoshiriki kufanya usafi na wananchi, alikuwa akitoa maagizo kwa wananchi kuacha kutupa taka ngumu hovyo na kuagiza Maafisa Afya na Mazingira kufuata sheria za mazingira kwa kutoa faini kwa wasiofanya usafi na kutupa taka hovyo.






# MATOKEO YA MASHINDANO YA AFYA NA USAFI MWAKA 2022

Dodoma

WIZARA ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara nyingine za kisekta hutekeleza mashindano ya afya na usafi wa mazingira kila mwaka.

Mwaka 2022, mashindano yalihusisha makundi 11; Halmashauri za Majiji (6), Manispaa (20), Miji (21), Wilaya (137), Vijiji (272); Hospitali za Rufaa za Mikoa za Serikali na Binafsi (37), Hospitali za Wilaya (99), Benki (25), Shule za Msingi (269), Shule za Sekondari (51) na Vyuo Vikuu (22).

Mchujo wa washindi ngazi ya taifa ulifanyika kati ya Julai-Agosti, 2022 ukitumia vigezo vya hali ya upatikanaji wa maji safi na salama, uwepo wa vyoo bora, udhibiti wa taka ngumu na majitaka.

Pia usalama wa chakula, upendezeshaji wa maeneo, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, utunzaji wa maeneo ya maziko, usimamizi wa sheria za usafi, ubora wa huduma za kijamii na usafi katika maeneo ya umma.

Vigezo vingine ni ubora wa huduma za usafi katika kuimarisha usafi na udhibiti wa taka, kuongeza upatikanaji wa majisafi na salama, kuboresha huduma za vyoo bora na vifaa vya kunawia mikono katika kaya, vituo vya kutolea huduma za afya, shule na taasisi nyinginezo.

Wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Usafi Kitaifa (Novemba16-19, 2022) na Siku ya Matumizi ya Choo Duniani Novemba19, 2022, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Seif Shekalaghe aliwatangaza washindi na kutoa zawadi zenye thamani ya shilingi milioni 200 kwa washindi wa mashindano hayo.

Dkt. Shekalaghe aliwatangaza washindi wa kwanza katika makundi 11 na kuwakabidhi zawadi kama ifuatavyo;

Kundi la Vyuo Vikuu - Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela na kupewa zawadi ya shilingi milioni moja.
Kundi la Benki - Benki ya NBC Dodoma na kupewa zawadi ya kombe na cheti.

Kundi la Hospitali za Wilaya - Hospitali ya Mugana, Missenyi na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milioni nne.

Kundi la Hospitali za Rufaa za Mikoa - Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Centre – Selian na kupewa zawadi kombe, cheti na shilingi milioni nne.

Kundi la Shule za Msingi - Shule ya Msingi Kimashuku iliyoko Wilaya ya Hai na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milioni nne.

Kundi la Shule za Sekondari- Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu iliyoko Geita na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milion nne.

Kundi la Halmashauri za Vijiji - Kijiji cha Image kilichopo Wilaya ya Njombe na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi laki tano.

Kundi la Halmashauri za Miji – Halmashauri ya Mji wa Babati na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milioni 15.

Kundi la Halmashauri za Manispaa - Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milioni 15.

Kundi la Halmashauri za Majiji - Halmashauri ya Jiji la Arusha na kupewa zawadi ya Kombe, cheti na shilingi milioni 15.

Kundi la Halmashauri za Wilaya - Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Mkoani Njombe na kupewa zawadi ya kombe, cheti na shilingi milioni 35.

Aidha, Dkt. Shekalaghe alieleza kwamba; "Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira yanaleta hamasa kwa wanaofanya vizuri kuendelea kufanya vizuri na wale wasioanya vizuri kwa mwaka 2022 wafanye vizuri zaidi katika mwaka ujao."

